# Ukaguzi wa ICE (Check-Ins): Unachohitaji Kujua

## MAMBO MUHIMU

- Ukaguzi wa ICE sio mahakama ya uhamiaji: Ukaguzi wa ICE umetenganishwa na usikilizaji wako wa mahakamani.
- Maafisa wa ICE hawatoi uamuzi wa kesi yako ya hifadhi au uhamiaji.

## UKAGUZI WA ICE NI NINI?

- Ni mkutano (ana kwa ana au kwa mtandao) na ICE wakati kesi yako bado inaendelea au kama una amri ya kuondolewa nchini.
- ICE hukagua:
- - Anwani yako
- - Kwamba huvunji sheria
- - Kwamba hujifichi au kuepuka mamlaka

## HATARI

- Baadhi ya watu wanaweza kukamatwa wakati wa ukaguzi:
- - Ikiwa wana amri ya kufukuzwa (deportation order)
- - Ikiwa wana rekodi za jinai
- - Ikiwa wamekiuka sheria za uhamiaji hapo awali
- - Hata kama hakuna haya yanayokuhusu, bado kuna uwezekano wa kukamatwa.

## VIDOKEZO VYA KUJIANDAA

- Leta:
- - Nakala za maombi yako yote ya uhamiaji na nyaraka zako
- - Ushahidi unaoonyesha muda uliokaa Marekani (kama bili za matumizi ya umeme, maji, n.k.)
- - Nyaraka zinazoonyesha hali maalum za kifamilia au kiafya
- Jaribu kwenda na rafiki au mwanafamilia ambaye ni raia wa Marekani na anayeongea Kiingereza.
- Kula kabla ya kwenda & vaa nguo za kustarehesha.
- Kumbuka namba muhimu za simu.
- Hakikisha wakili wako na watu unaowaamini wana maelezo yako kamili kama vile: “ nambari ya A ” , tarehe ya kuzaliwa, jina kamili, na nchi unakotoka.

## IWAPO UTASHIKILIWA

- Waambie maafisa wa ICE wazi na mara kwa mara:
- “ Ninaogopa kurudi nchini kwangu na nataka kuomba hifadhi. ”
- Hii inapaswa kusababisha Mahojiano ya Hofu Inayokubalika (Credible Fear Interview).

## MASHARTI

- Ukipokea “ Notisi ya Kuripoti ” (Notice to Report), tafuta ushauri wa kisheria.
- Kukosa kufika kwenye ukaguzi wako wa ICE kunaweza kusababisha kukamatwa au kufukuzwa nchini.

## UKIKOSA UKAGUZI WAKO

- Wasiliana na ICE na eleza sababu ya kukosa miadi.
- Wasiliana mara moja na wakili wa uhamiaji.

## USHAURI WA JUMLA

- Ongea na wakili wa uhamiaji kabla ya kwenda.
- Beba nyaraka zako za uhamiaji.
- Nenda na mtu wa kukusindikiza.
- Usisaini kitu chochote ambacho hujakielewa.